TANGAZO LA SERIKALI NA. 548 la tarehe 5/7/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA MWAMBESI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Mwambesi ya Mwaka 2024.

Tangazo

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Mwambesi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA YA TUNDURU


MSITU WA HIFADHI YA MAZINGIRA ASILIA MWAMBESI

*Makadirio ya Eneo:* Hekta 112282.98 au Kilometa za Mraba 1122.829

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la ardhi awali likijulikana kama Msitu wa Hifadhi wa Taifa Mwambesi linalopatikana Wilaya ya Tunduru, Mkoa wa Ruvuma lenye ukubwa wa takribani Hekta 112282.98 au Kilometa za Mraba 1122.829 kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2765 ya mwaka 2018 (Skeli 1:200,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikal Na. 548 (Linaendelea)*




Dodoma, ANGELLAH JASMINE KAIRUKI

___24 Mei, 2024 *Waziri wa Maliasili na Utalii*